**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Monday 10 May 2004 (afternoon)
Lundi 10 Mai 2004 (après-midi)
Lunes 10 de mayo de 2004 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.

*Kifafanue kimoja kati ya vifungo vifwatavyo:*

**1.** (a)

Punde jua litazama    na giza litagubika
Punde shughuli ‘takoma    hili zogo na pirika
Punde tuliyoyachuma    yataanza ‘hesabika
Punde vitaporomoka    mwanzo vilivyosimama.

Punde vilivyotuwama    vitaanza ‘tikisika
Punde vilivyoinama    hima hima ‘tainuka
Punde vilivyosakama    ‘taona vyasakamuka
Punde muda utafika    na utafika lazima.

Punde wagonjwa wa homa    kwinini zitawafika
Punde pumu zinopuma    ‘tapowa ‘tashuwarika
Punde vichwa vinouma    moto havitatuwaka
Punde tabibu ‘tazuka    na maradhi ‘talalama.

Punde bubu atasema    fasaha wa kusikika
Punde ‘takwenda kilema    mabio atatimka
Punde kipofu ‘tasoma    na hati ataandika
Punde kweli itawaka    na uongo utazima.

Punde punda atagoma    na zigo kulikanuka
Punde wanaomtuma    ndio wataotumika
Punde wanaosukuma    ndio wataoanguka
Punde pindu ‘tapinduka    aliyedhani yu wima.

Punde ngoma inovuma    yenyewe itapasuka
Punde boso litazima    duara kutawanyika
Punde nyimbo itakoma    malenga ataondoka
Punde walioalika    nyuso zitawaparama.

Punde ‘tashindwa kusema    hata kama sikutaka
Punde ‘tashindwa lalama    nipaswapo lalamika
Punde hapa nitahama    mgeni nitaoneka
Punde yatathibitika    yote niliyoyasema!

Kutoka *Mawiyo*, Mswada wa Mohamed Ghassany, 2003

- Mshairi anajaribu kutwambia nini katika shairi hili?
- Mbali na arudhi, mbinu gani kuu zinazotawala katika shairi hili?
- Kwa kiasi gani mbinu hizi zimefaulu kuwasilisha mawazo ya mshairi na kwa taathira gani?
- Kwa namna gani unafarajika au unakatishwa tamaa na fikra na falsafa ya mshairi huyu?

**1.** (b)

Mheshimiwa mmoja maarufu sana mwishoni mwa wiki moja anafika nyumbani majira ya usiku wa manene na kukuta kufuli mbili zimebanwa penye mlango wa chumba chake huku ameburuana na kisura.

Kufuli ya kwanza ni ile yake mwenyewe mpangaji na ya pili ni ya mwenye nyumba ambayo ameifunga kwa kuwa jamaa huyu amechelewa kulipa kodi ya nyumba kwa muda wa miezi minne mfululizo. Na kodi ya mwezi mmoja ni shilingi mia sita hamsini.

Katika matembezi yangu napita mtaa anakoishi jamaa huyu. Siku yenyewe ni nono maana baada ya kupata donge anafululiza moja kwa moja hadi nyumbani. Anavalia suti mtindo mamboleo na kushikana na kisura mmoja maridadi na kuelekea mjini kwenda kujistarehesha sinema.

Wakati wa usiku baada ya shamrashamra zao, wakiwa wamejaa furaha za starehe, wanarejea nyumbani. Mheshimiwa na kimwana wameshikana mikono. Hamad! Kufika tu kwenye chumba anakuta kufuli mbili zimefungwa. Badala ya lile lake kuna lingine kwenye kipete cha mlango. Jasho linaanza kumchiririzika. Akili zimemruka maana kipusa anaye na huku kufuli mbili zimebana pale mlangoni.

Kwa bahati, jirani yake mmoja anamsikia akinung'unika. Anamjia na kumweleza kwamba aliyebana kufuli ya pili ni mwenye nyumba. Kwa hamaki mheshimiwa anaanza kufokwa na maneno na mwisho anamwendea mwenye nyumba ambaye chumba chake kiko nyuma ya jengo hili.

Anamwamkua na kumtafadhalisha amfungulie chumba lakini mwenye nyumba anakuja juu kama mbogo. Ikawa ni aibu kutiana ngumi mbele ya kisura na umati mkubwa ulioanza kusongamana. Wakati huo, mwenye nyumba anashikilia lazima alipwe kodi ya miezi minne ama sivyo, "hata akija nani sifungui," anashikilia mwenye nyumba.

Zogo linaendelea kumcheka. Mheshimiwa anakuja juu naye mwenye nyumba anachemka kama maji ya moto. Nusra washikane. Lakini, kwa bahati majirani pamoja na wengine tulioko kando tunaamua ugomvi.

Mheshimiwa akaokolewa kwa kupewa ufunguo kwa masharti kwamba asipolipa kodi kwa muda wa siku saba, atakuta kufuli zaidi. Lakini ingawa kafunguliwa mlango, aibu imejaa mbele ya kisura wake.

Kutoka *Kichaa cha Pesa* na R. Muthusi, 1977

- Katika kisa hiki mwandishi anajaribu kusema nini?
- Vipi mtindo na mbinu alizoutumia mwandishi zinamwezesha kusema anachotaka kusema na kwa taathira gani?
- Dondoo hili linahusianaje na maisha yalivyo katika miji ya Afrika ya Mashariki?
- Zungumzia mbinu ya usimulizi nafsi ya kwanza kama kipengele muhimu kufanikisha au kutofanikisha kisa hiki?